

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: Na. 027-2660501

Fax: Na. 027-2660500

Barua pepe: Info@mkingadc.go.tz

Tovuti: www.mkingadc.go.tz



S.L.P. 6005,
TANGA.

KUMB.NA. HW/MKG/D.36/245/71

Tarehe 11/07/2024

TANGAZO

(Limetolewa chini ya Kifungu cha 155(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 Rejeo la Mwaka 2002 la Sheria za Tanzania.

Wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga mnatangaziwa kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria Ndogo ifuatayo:

1. Sheria ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ya Mwaka 2023 na marekebisho yake .

I) CHIMBUKO LA SHERIA NDOGO HIZI NI:

- a) Kifungu cha 7(1), na 16(1) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290.
- b) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga za Mwaka 2019 ambazo zilichapishwa katika Tangazo la Serikali namba 877 la tarehe 15/11/2019.

II) MADHUMUNI YA SHERIA NDOGO HIZI

- a) Kuboresha na kuhuisha viwango vya ada na ushuru vilivyowekwa na Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Mwaka 2023 na marekebisho yake.

III) MAMBO MUHIMU YATAKAYOZINGATIWA KATIKA SHERIA NDOGO HII


Katika Marekebisho ya Sheria ndogo hizi Halmashauri imezingatia mapendekezo na maoni ya wadau juu ya mabadiliko ya vipengele vichache vilivyopo katika sheria hii hasa tozo za maroli na tozo za dagaa ,Pamoja na matakwa ya sheria mama ili kuepuka kukinzana pamoja na hali halisi ya kiuchumi ya wakazi na wafanyabiashara wakubwa na wadogo wanaofanya shughuli zao katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.

IV) MATOKEO YA KUTUNGWA KWA SHERIA NDOGO HIZI

- a) Kuwezesha Halmashauri kukusanya mapato yake kwa kuzingatia taratibu za kisheria,
- b) Kugharamia shughuli za miradi ya maendeleo
- c) Kuongeza mapato ya Serikali pamoja na ya mtu mmoja mmoja na wafanya bisahara kwa ujumla

Watu wote ambao kwa njia moja au nyingine wataathiriwa na Sheria Ndogo hizi wanakaribishwa kuleta maoni yao juu ya Sheria Ndogo hizi ndani ya muda wa siku 30 tokea tarehe ya tangazo hili. Maoni yanatakiwa yawasilishwe kwa maandishi katika ofisi za Kata au Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.

Nakala za Rasimu za Sheria Ndogo hizi zinapatikana katika Ofisi za vijiji, Kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kitengo cha Sheria.



RASHID K. GEMBE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

Nakala:

1. Mkuu wa Wilaya
Wilaya ya Mkinga
2. Mwenyekiti wa
Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga
3. Mbao za Matangazo

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

**Ofisi za Kata
Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga**

4. Mbao za Matangazo
**Ofisi za Vijiji
Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga**
5. Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga
6. Taasisi Wadau
Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga
7. Mitando ya Kijamii (Mkinga yetu)
Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga